©Haki Milki

Kitabu hiki kimeandaliwa na Mwl. Malosha, Januari, 2023. Haki zote zipo chini ya ya ©Mwl. Malosha.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kudurufisha, au kuhamishwa kwa namna yoyote au kwa njia yoyote, kielectroniki au kiufundi, ikiwepo kupiga fotokopi, kurekodi au kwa namna yoyote ya kuhifadhi au kurudishia tena, bila idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi.

Kufanya hivyo ni kuvunja sheria na haki ya mwandishi na mchapishaji, na ukiukwaji wa utaratibu. Hii inaweza ikapelekea mashtaka kutoka kwa waandaaji wa kitabu hiki.

**ISBN: 235 – 5587 – 550 – 57 – 9**

**Mawasiliano:**

Simu: 0762129917 / 0762129917

WhatsApp: 0762129917

Instagram: @Disciple Malosha

Facebook Page: @ Brothers Malosha Brothers Malosha

E-mail: mmalosha921@gmail.com

**Kimehaririwa na KalamuSmart na kupigwa chapa na Malosha Publishers (MP Design & Printing)**

**0762129917 / 0763150015.**

**Katoro - Geita.**

# YALIYOMO

**SHUKRANI**……………………………………………………………………………………iii

**UTANGULIZI**…………………………………………………………………………………iii-iv

**SURA YA KWANZA**………………………………………………………………………………1

Naye Yabesi Alikuwa Mwenye Heshima………………………………………………………1-2

Mama Yake Akamwita Jina Lake Yabesi……………………………………………………………3

Mungu Hakubadili Jina La Yabesi Alibadili Kesho Yake……………………………………………4

Mungu Alitumia Huzuni Ya Yabesi Kama KIBEBEO Cha Kumpa Furaha………………4-5

Ukitaka Kufanikiwa Kimaisha Kubali Kwenda Kinyume Na Mazoea……………………5-6

Yabesi Akamlingana Mungu Wa Israeli…………………………………………………………7

**SURAYA PILI**………………………………………………………………………………………8

Sayansi Ya Maombi Ya Yabesi……………………………………………………………………8-9

Yabesi Alikuwa Mtu Wa Kawaida Miongoni Mwa Watu Wa Kawaida………………9-10

Unyenyekevu Wa Yabesi Ulitengeneza Maombi Binafsi Ya Kimkakati……………11-13

Lau Kwamba Ungenibariki Kweli Kweli…………………………………………………13-14

Mungu Haangalii Umeanzaje Anaangalia Unamalizaje……………………………………15

Yabesi Hakuomba Maombi Ya Kulalamika, Lakini Habakuki Aliomba Maombi Ya Kulalamika…………………………………………………………………………………………16-17

Kunizidishia Hozi Yangu……………………………………………………………………17-18

Mwombaji Ni Chombo Cha Dola Ya Mbinguni……………………………………………18

Mkono Wako Ungekuwa Pamoja Nami…………………………………………………19-20

Kiwango Chako cha Nguvu za Mungu Kinategemea Kiwago Chako cha Maombi……20

Nawe Ungenilinda Na Uovu……………………………………………………………………21

Ili Usiwe Kwa Huzuni Yangu……………………………………………………………………22

Jifunze Kuwaombea Wengine…………………………………………………………………22

**SURA YA TATU**……………………………………………………………………………………………24

Majibu Ya Mungu Ni Yapi………………………………………………………………………………24

Maswali Yako Kwa Mungu Ni Yapi…………………………………………………………………24-25

Naye Mungu Akamjalia Hayo Aliyoyaomba…………………………………………………24-25

Majibu Yako Kwa Mungu……………………………………………………………………………26

# SHUKRANI

Ninamshukuru MUNGU kwa neema hii ya kuandaa kitabu hiki kinachosema "MAOMBI YA YABESI" nitoe shukrani zangu kwa **Mch. Emanuel Sengo** kwa kutoa masomo mbalimbali katika Parishi ya Katoro Tumaini. Namshukuru MUNGU kiwepo mikononi mwako na MUNGU ni mwaminifu mno kajidhihirisha mno! Shukrani zangu kwa familia yangu, mke wangu mpenzi **Angel Malosha** kwa kuniombea kuwa na maisha ya kuukulia wokovu kwa kunishauri na kunitia moyo katika kila hatua. Shukrani zangu kwa timu ya maombi ya **AICT TUMAINI** chini ya Mtumishi **Richard** katika huduma na malezi ya kiroho na ushauri, bila kumsahau mke wake Pastor **Sengo Emanuel** kwa kazi yenu njema ya kutulea.

MUNGU AWABARIKI SANA

Mwandishi.

# UTANGULIZI

Kitabu hiki cha Maombi ya Yabesi ni kitabu kitakachokupa mwongozo mzuri wa namna ya kuomba maombi binafsi, kama kuhani wa familia, kanisa, nchi na hata katika ngazi yoyote ile uliyonayo. Maombi ya Yabesi ni maombi yaliyokaa katika mfumo wa kuomba binafsi. Lakini pia wachambuzi mbalimbali wa Theologia na wanazuoni mbalimbali wanakinzana juu ya maombi kama haya, wanasema maombi ya ubinafsi (self prayer), lakini ikumbukwe kuwa unapoomba maombi yako binafsi unapovuka au usipovuka ni vyema kuwaombea wengine pia "*imetupasa sisi tulio na nguvu kuuchukua udhaifu wao wasio na nguvu, wala haitupasi kujipendeza wenyewe (Rumi 15:1).*

Hapa anazungumzia kuwaombea wengine wenye shida mbalimbali, Yabesi alihitaji kuvuka kwanza yeye katika Wana wa Yuda, hivyo historia ya ukoo wake ilikuwa mbaya ukilinganisha ukoo wake wote walizaa na kufa bila hata kufanya maombi ya kimkakati kama aliyoyafanya Yabesi. Mfano ukiangalia ukoo wake utaona yako majina ya wanaume kadhaa walizaa watoto na watoto wao nao wakazaa na wakafa na hatujui hao waliokufa. Kuna wengine waliokufa na umasikini, utasa, migogoro ya ndoa, kufeli, laana, huzuni na kutokupanuliwa kwa mipaka yao. Unaweza kuniuliza swali, mtumishi umejuaje haya?

Angalia mwenyewe ilipofika kwa mtu ambaye hayo yote ameyaona kweye kabila na ukoo wake yamekuwa changamoto hakukubali tu kufa na hali iliyozoeleka kwenye ukoo wake--Yabesi hakukubaliana na historia ya Wana wa Yuda kwenye maisha yake. Kumbuka, "**Shetani hutubania kwenye historia za maisha yetu",** kwamba fulani alishindwa sembuse wewe? Lazima kuwe na akina Yabesi wanaobadilisha leo yao mbaya na kuwa kesho yao nzuri. Ndiyo maana ilipofika kwa mtu anayeitwa Yabesi hadithi ya Sura nzima ya kitabu cha Mambo ya Nyakati ilibadilika, unasema ilibadilikaje? Biblia inasema ilipofika zamu yake "*Huyo Yabesi akamlingana Mungu wa Israeli...(1Nyakati 4:10 )***. "KUMLINGANA "**Maana yake ni kumwomba Mungu, kumusihi Mungu kwa maombi, kumlilia Mungu kwa maombi au kuutafuta uso wa Mungu kwa njia ya maombi.

Yabesi alihitaji msaada wa maombi juu ya kilio alichokuwa nacho cha muda mrefu kama vile Daudi alivyosema *"Ee BWANA, usikie kuomba kwangu, kilio changu kikufikie*

*(Zaburi 102:1).”* Mungu alisikia kilio cha huyo Yabesi na akabadilisha historia yake japo kabila lake kuna watu hawakuonekana kuwa wamefanya mabadiliko. Yabesi hakujidharau , alijikubali na aliamini Neno jema laweza kutoka kwake hata kama wazawa wa Yuda na wazawa wa kabila la Simeoni hakutokea mtu aliyeamua kuomba .Yabesi aliomba; maandiko matakatifu yanasema "...*Naye Mungu akamjalia hayo aliyoyaomba (1 Nyakati 4:10)."*

Ezra kuhani mwandishi wa sheria na mfundishaji, wakati anaandika kitabu hiki cha Mambo ya Nyakati kilikuwa ni kipindi cha Yoshua, wakati huo wanatoka uhamishoni Babeli. Yabesi alikuwa ni mmoja wa kabila la Yuda, ikumbukwe kwamba taifa la Israeli lilikuwa na jumla ya makabila kumi na mawili (12), sawa na wana wa Jakobo; mfano Reubeni, Simeoni, Lawi, Yuda, Isakari, Zabuloni, Yusufu, Benyamini, Dani, Naftari, Gadi na Asheri; na kila kabila lilikuwa na kazi yake. Nitatoa mifano michache; baadhi ya makabila, mfano kabila la Lawi walikaa madhabahuni kuhudumu na kuimba na tunaona kazi yao ilikuwa ni kuimba na kusifu na kila kabila la Israel lilikuwa na asilimia kadhaa ya Walawi. Ikumbukwe kuwa Musa alikuwa ni Mlawi jambo ambalo Walawi wengi walihusika kusimamia sheria za Mungu kwa kutoa sadaka na kuhudumu madhabahuni kama kusifu na kuabudu--leo hii tunaita ‘praise and worship team’.

"*Tena Walawi waimbaji, wote pia, yaani Asafu, na Hemani, na Yeduthuni, na wana wao, na ndugu zao, hali wamevaa kitani safi, wenye matoazi na vinanda na vinubi, wamesimama upande wa mashariki wa madhabahu, na pamoja nao makuhani mia na ishirini wakipiga panda (2 Nyakati 5:12).* Hawa Walawi walishusha uwepo mpaka makuhani hawakuweza kuhudumu hiyo ilikuwa kazi yao. Pia wana wa Isakari, hawa jamaa walikuwa na akili sana na wenye kujua nyakati na nini Israeli wafanye, "*Na wa wana wa Isakari, watu wenye akili za kujua nyakati, kuyajua yawapasayo Israeli wayatende; vichwa vyao walikuwa watu mia mbili na ndugu zao wote walikuwa chini ya amri yao (1 Mambo ya Nyakati 12:32-34)."*

Ukisoma utaona kila kabila lina kazi zake ni sawa na kusema hapa kwetu Tanzania tuna zaidi ya makabila 120 na kila kabila lina kazi yake na tamaduni zake; kama ni Wamaasai tunaona ni wafugaji, Wasandawe na Wahanzabe ni wawindaji, na makabila mengine mengi na ndivyo ilivyokuwa katika taifa la Israeli. Pia tunaona katika kitabu cha 1 Nyakati 4:1-23 kuwa ni uzao wa Yuda na waliozaliwa wametajwa hapo kuwa *Wana wa Yuda; Peresi, na Hesroni, na Karmi, na Huri, na Shobali;* na ukisoma tena huo uzao wa Yuda ambapo Yabesi alitokea tunakuja kuona uzao unakua mpaka anakuja kutokea mwokozi Yesu Kiristo katika agano jipya. "*Yuda akamzaa Peresi na Zera kwa Tamari; Peresi akamzaa Esromu; Esromu akamzaa Aramu;.. (Mathayo 1:3 )*.

Yabesi wa Agano Jipya ndiyo huyo huyo wa Agano la Kale maana katika Agano la Kale. Tumeona, **"***Wana wa Yuda ni Peresi...(*1 Nyakati 4:1). "Na tunakuja kuona tena katika agano jipya, *"Yuda akamzaa Peresi ...(Mathayo 1:3). "*Kwa hiyo Yuda alikuwa ni mbegu wa kuja kumtoa mpaka Masihi aitwaye Yesu Kristo. Kitabu hiki unachokisoma, kuna kitu Mungu atasema na wewe kwa habari ya Maombi ya YABESI na hautabaki kama ulivyozoea.

Maombi ni mawasiliano ya Kiroho kati ya mwanadamu na Mungu au kati ya mwanadamu, na miungu. Wakati mwingine maombi yanaweza yakawa siyo maombi tena; wakati mwingine ni vita baina ya mwombaji na aliyemiliki kitu au vitu vya mwombaji. Mfano, shetani aliyeiba mali, ameiba afya lazima kuomba kwa namna ya maombi ya vita maana shetani kazi zake ni **KUIBA, KUCHINJA** na **KUHARIBU** na hapa hakuna cha mawasiliano tena ni vita kulazimishana atoe alichomiliki (maombi ya vita) na vita ili iwe vita lazima ihusishe SILAHA. Kama mkiristo kuna silaha za kupigana na shetani katika ulimwengu wa roho. Paulo, anasema katika "W*aefeso 6:11, Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani."* Swali, ni silaha zipi? Paulo amezitaja katika kile kitabu cha (Waefeso 6:13-17); dirii ya haki, Injili ya amani, ngao ya imani, upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu.

Kumbuka maombi ni sayansi kwa maana ya kila mara yanabadilika, kwa hiyo tambua ulimwengu tulionao shetani anatumia mbinu mbalimbali kudhoofisha wakristo ili wasiombe. Kwa neema ya Mungu kitabu hiki kitakupa mwanga mkubwa juu ya kujitegemea wewe kama mwombaji, na mabadiliko yaliyopo katika ulimwengu wa roho juu ya kuomba, kama vile ulimwengu hapo mwanzo ulikuwa unatumia analogia kupata habari na kwa sasa tupo dijitali; vivyo hivyo shetani naye ana mbinu zake katika ulimwengu wa roho.

Kumbuka, Yesu tangu afe msalabani hajabadilika; upako wa msalabani uliovunja pazia la hekalu, uliosababisha makaburi yakafumuka, ulioleta giza masaa matatu, uliotetemesha nchi, bado ni yuleyule hajabadilika. *"Yesu Kristo ni yeye yule, jana na leo na hata milele (Waebrania 13:8). "*Pamoja na kwamba habadiliki yeye ni Bwana wa mabadiliko; anabadilisha majira ya umasikini na kuwa utajiri anabadilisha majira ya laana na kuwa baraka" **…***kuwa nimekuwekea mbele yako uzima na mauti, baraka na laana; basi chagua uzima, ili uwe hai, wewe na uzao wako. (Kumbukumbu la Torati 30:19 ).* **"**Uchaguzi huu wote uko katika kuomba, katika kuomba waweza omba vizuri au vibaya, kumbuka ukiomba vibaya utapata matokeo mabaya na ukiomba vizuri utapata matokeo mazuri kama aliyoyapata Yabesi.

Mzee Yakobo anasema katika Yakobo 4:3, Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu. Ni hatari sana kwa mwombaji

ukaomba kitu kwa Mungu, halafu ukatumia nafasi hiyo vibaya. Sijajua daraja la uombaji wako maana kuna waombaji wa familia, waombaji ngazi ya Kanisa, waombaji ngazi ya ukoo; kuna waombaji ngazi ya taifa, lakini pia kuna waombaji ngazi ya kidunia. Sasa lazima utambue upo nafasi gani kama kuhani wa maombi. Samweli alitambua nafasi yake ya maombi mpaka akasema, kwa sababu nimepewa nafasi ya kuombea taifa la Israeli, alipoona kuna dalili za kuacha kuomba akawambia Israeli "*Walakini mimi, hasha! Nisimtende Bwana dhambi kwa kuacha kuwaombea ninyi; lakini nitawaelimisha katika njia iliyo njema, na kunyoka (1 Samweli 12:23)".* Angalia hilo neno 'Nisimtende Bwana dhambi..'. Ni dhambi kubwa sana kama umebebeshwa mzigo na Roho Mtakatifu wa kuombea nchi, au familia au kanisa, au kitu chochote halafu ukakaa tu unajiita mwombaji.

Kumbuka "**Maombi ni Kazi".** Kama wewe ni mwalimu tunasema ualimu ni kazi kama kazi zingine. Sasa unapokuwa mwombaji wewe ni mwajiriwa katika ufalme wa Mungu, katika kitengo cha mizinga, mabomu, maguruneti, zima moto, nk. Ofisi yako inatambulika kama OFISI YA MAOMBI. Katika ofisi yako lazima utambue maadui wana silaha zipi--kwa lugha nyingine wewe ni MLINZI unalinda malango ili maadui wasipenye katika ufalme wa Mungu. Kazi yako ni kuwahubiri wanyenyekevu habari njema, kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao kwa sababu wewe ni mlinzi. Biblia inasema kwamba *"Nimeweka walinzi juu ya kuta zako, Ee Yerusalemu; hawatanyamaza mchana wala usiku; ninyi wenye kumkumbusha Bwana, msiwe na kimya(Isaya 62:6)".* Mlinzi anayetajwa hapa ni wewe!

"**MWOMBAJI NI MLINZI".** Walinzi wanatofautiana; wapo wengine hawalali wengine akiingia lindoni anachukua kigodoro chake analala huyo siyo mlinzi; ni mlalaji anayebadilisha mazingira ya nyumbani na kwenda kulala kwingine. Nabii Isaya mwana wa Amozi anasema, mwombaji asiyelala usiku wala mchana. Mungu akupe neema ya kukisoma kitabu hiki maana wewe ni bora Mungu amekuona miongoni mwa wengi ili upate kujifunza juu ya **MAOMBI YA YABESI** katika ulimwengu wa roho. Wewe ni muhimu sana umetoka miongoni ili utengeneze mahali palipobomoka, "*Nami nikatafuta mtu miongoni mwao, atakayelitengeneza boma, na kusimama mbele zangu mahali palipobomoka, kwa ajili ya nchi, nisije nikaiharibu, lakini sikuona mtu (Ezekieli 22:30)"*

**Karibu sana mpendwa msomaji wangu!**

## SURA YA KWANZA

**MAMBO MUHIMU ISHIRINI (20) YALIYOMO KATIKA KITABU (1 NYAKATI 4:9-10)**

**"***Naye Yabesi alikuwa mwenye heshima kuliko nduguze; na mamaye akamwita jina lake Yabesi, akisema, Ni kwa sababu nalimzaa kwa huzuni Huyo Yabesi akamlingana Mungu wa Israeli, akisema, Lau kwamba ungenibarikia kweli kweli, na kunizidishia hozi yangu, na mkono wako ungekuwa pamoja nami, nawe ungenilinda na uovu, ili usiwe kwa huzuni yangu! Naye Mungu akamjalia hayo aliyoyaomba". (1 Mambo ya Nyakati 4:9 -10)*

Katika mistari hii miwili itatusaidia kujua hayo mambo ishirini (20) hebu tuyaangalie hayo mambo:

### 1. "Naye Yabesi Alikuwa Mwenye Heshima Kuliko Nduguze"

"*Naye Yabesi alikuwa mwenye heshima kuliko nduguze..." (1 Mambo ya Nyakati 4:9)*. Katika Yuda yote na uzao wa wana wa Yuda hatujaona mtu kaandikwa alikuwa mwenye heshima isipokuwa YABESI. Heshima inayoongelewa hapa ni kama vile mtu kaalikwa kwenye sherehe na kila mtu anamtegemea kwa nafasi aliyonayo kwamba atasema neno ndiyo tunaita **Mgeni Rasmi.** Ndiyo heshima anayopewa YABESI. Hatujaambiwa heshima ilitokana na nini maana mtu anaheshimiwa katika jamii kwa elimu, utajiri, siasa na vitu vingine vingi.

Biblia inaniambia aliheshimiwa na kaka zake, dada zake na ndugu wote. Heshima aliyokuwa nayo ilikuwa ya mwilini, "**Heshima ya mwilini haitengenezi mazingira ya kuheshimiwa rohoni".** Kuwa mzee wa miaka mingi kimwili haimaanishi umekuwa mzee wa rohoni. Inategemea umeanzia rohoni au mwilini. Chochote kile unachokiona mwilini kimeanzia rohoni; unaweza ukaheshimiwa mwilini na ukadharauliwa rohoni kama Yabesi. Ndiyo maana Yabesi aliona ile kwamba watu wanamweshimu kimwili, wanampigia makofi, wanamsifia sana hakubweteka na heshima za kibinadamu ilibidi atafute heshima kubwa KULIKO zote ya kuheshimiwa na Mungu kwa njia ya kuomba. "**Hakuna mtu aliyewahi kuvuka (kutoboa) duniani bila kutafuta Heshima ya Mungu kwa njia ya maombi"**

Yabesi alitaka kutumika kwa njia ya Maombi Binafsi (Self Prayers) "*...mtu akinitumikia, Baba atamheshimu (Yohana 12:26). "*Yabesi alihitaji Heshima ya Mungu kwa kutumika kwa njia ya maombi**. "Shetani haogopi Mchungaji, Nabii, Askofu, Mwijilisti au mtu yeyote, bali anaogopa Mwanamaombi. Kumtumikia Mungu bila maombi ni sawa na kuendesha gari bila mafuta"** ile kwamba unaimba vizuri, unahubiri vizuri, wewe ni Askofu, Mchungaji, Mzee wa kanisa, kiongozi yeyote wa kanisa haina maana kuna vitu viko sawa. Yamkini unatumika vizuri na kupewa heshima kama Yabesi, yamkini kumbe kuna mahali unakwama unahitaji Heshima ya kiMungu zaidi Mungu akuheshimishe. Kwa njia ya maombi kama Yabesi tafuta uso wa Mungu kwa njia ya maombi binafsi maana, ukimtafuta BWANA, maadamu anapatikana, ukimwita maadamu anaitika, anasema; niite nami nitakuitikia, nami nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua.

Yabesi hakuangalia heshima aliyokuwa nayo aliangalia uzito wa jaribu lake la kutokuvuka maana **"Ukubwa wa Baraka Yako ndiyo Ukubwa wa Jaribu lako"**. Ndiyo maana Mungu haangalii heshima uliyonayo, bali anaangalia moyo wa kumtafuta Bwana. Yabesi alikuwa mtu mwenye heshima na akaomba maombi ya heshima na akapata matokeo ya heshima mbele ya watu wenye heshima.

Yabesi hakutaka heshima kwa nduguze, alitaka heshima ya kiMungu. Ukitaka kuheshimiwa mwombe mwenye heshima maana heshima na adhama zina yeye. Neno 'Adhama' maana yake **"Utisho".** Yabesi hakuwa na maarifa ya rohoni alikuwa na heshimu ya kibinadamu, hivyo alifanana na wanyama wapoteao "*Mwanadamu mwenye heshima, iwapo hana akili, Amefanana na wanyama wapoteao Zaburi 49:20*". Haijalishi unaheshima KULIKO ndugu zako, unaheshimiwa kazini au mahali popote, **"Heshima uliyonayo ndiyo iliyobeba vita yako"**. Heshima ya Rais ndiyo iiyobeba vita yake, ndiyo maana utaona ana ulinzi masaa yote. Ukitaka heshima mbele za Mungu kilinde ulichonacho kwa maombi maana si wote wanapenda uwe hivyo. Shika sana ulicho nacho, asije mtu akaitwaa taji yako.

## 2. "Mamaye Akamwita Jina Lake Yabesi"

"*...na mamaye akamwita jina lake Yabesi Kwa sababu nalimzaa Kwa huzuni" 1 Mambo ya Nyakati 4:9b*". Hii familia ya akina Yabesi na kaka zake na dada zake hapa hatuoni baba wa familia. Inawezekana huyu mama ndiye alikuwa baba ndiye alikuwa mama. Kila kitu kilimuangalia yeye, yamkini aliishi kwa mateso kama mama mjane asiye na msaidizi ndiyo maana tunaona anachukua mimba na kumzaa mtoto angalia jina analomwita linasadifu mazingira ya mateso aliyoyapitia wakati wa ujauzito wake yawezekana magonjwa, uchungu, kuumizwa, njaa na mateso mengine mpaka

mamaye anamwita jina la Yabesi likiwa limebeba mateso, huzuni na maumivu. Pamoja na mateso hayo Yabesi alipoomba Mungu alimwokoa nayo yote*" Mateso ya mwenye haki ni mengi, Lakini BWANA humponya nayo yote. (Zaburi 34:19)".*

Katika tamaduni za Kiafrika kila familia ina jina lake la ukoo huo na hilo jina linakuwa na maana mfano jina la Nupanga lililotokana na Ngabaka linalotumika sana kusini magharibi mwa Kongo likiwa na maana 'Dunia imekuwa chungu.' Pia wazazi wengi wa Kiafrika wamekuwa wakiita majina mbalimbali ya wazee, matukio wakati mtoto anazaliwa mfano wakati wa jua kali mtoto unamwita "Lemi" ikiwa na maana ya 'Jua' kwa lugha ya Kisukuma na Kihaya 'Izobha'.

Pia katika Biblia kuna majina ambayo wazazi waliwapa watoto wao na yakabadilika, mfano Yakobo akawa Israel, Abramu akawa Abrahamu, Sarai akawa Sara, Sauli akawa Paulo, Beltashaza akawa Danieli, Hanania akawa Shadrack, Mishael akawa Meshack, Azaria akawa Abedinego, majina ambayo hayakubadilika na bado watu walifanikiwa kiroho na kimwili. Tabitha yule Dorkasi wa kitabu Cha Matendo 9:36 na mwanafunzi mmoja alikuwako Yafa, jina lake Tabitha, tafsiri yake ni Dorkasi (yaani paa); mwanamke huyu alikuwa amejaa matendo mema na sadaka alizozitoa. Hilo jina likiwa na maana ya paa yaani swala. Wapo ambao walibaki na majina yao lakini bado hawakubadilika mfano, Nabali kama jina lake lilivyo ndivyo alikuwa likiwa na maana ya mpumbavu.

Kadhalika, mtoto anaweza akawa na jina lenye tafsiri isiyo njema, lakini kama atakuzwa katika njia sahihi, hiyo haimzuii Mungu kumtumia, na jina lake kufanya kusudi lake tunaona Yabesi jina lake likiwa na maana ya" HUZUNI" haikumzuia Mungu kufanya jambo lake la kiagano. Kumbuka "**nyuma ya jina kuna roho"**. Fikiria mtu anaitwa Bulemela yaani mtu mvivu; Matugandama yaani masikio ya ndama au Mayala yaani njaa; haina maana utaliishi hilo jina, kama utalikana kwenye ulimwengu wa roho. Kwa maombi kama Yabesi maana hakukubali yeye ni mtu wa huzuni japo aliitwa huzuni kwa maana Yabesi hakuliishi alichukua hatua ya kuomba na kukubali mabadiliko.

## 4. "Mungu Hakubadili Jina la Yabesi, Alibadili Kesho Yake"
## "Mungu Habadiliki ila Yeye ni Mungu wa Mabadiliko"

(God does not change but He is the God of Changes)

"*Yesu Kristo ni yeye yule, jana na leo na hata milele Waebrania 13:8"* . Habadiliki ila anabadilisha mambo, alibadilisha huzuni ya Yabesi ikawa kicheko kutokana na kuomba

kwake kwa bidii "...*Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii (Yakobo 5:16*)". Mama yake na Yabesi alitengeneza kesho yake ilivyokuwa inabeba jina lake lakini ashukuriwe Mungu Yabesi alipoomba (kumlingana) Mungu alibadili kesho yake.

Unaweza ukawa na jina zuri lakini usibadilike au usifanikiwe na ukaenda jehanamu. Hapa simaanishi uitwe jina lolote kama malaya, kahaba na mwizi kama jina lako linabeba uhalisia usio mzuri . Kataa kwa jina la Yesu na kama ni zuri lisadifu uhalisia wake. Utakapoifahamu kweli ndiyo itakuweka huru siyo jina lako ni kweli tu ya Neno la Mungu katika Kristo YESU.

## 5. Mungu Alitumia Huzuni ya Yabesi Kama Kibebeo cha Kumpa Furaha

Unaweza usinielewe vizuri. Ngoja nikupe mfano, nimekuja kwako nina kiu ya maji ya kunywa, utanipa maji kwa KIBEBEO kipi? Jibu ni kikombe. Kwa hiyo umetumia kikombe kama KIBEBEO cha maji kuondoa kiu yangu! Hivyo, ili Mungu afanye jambo kwako nenda mbele za Mungu na kibebeo kama chombo au daraja la muujiza wako. Haleluyah!! Mungu hutumia huzuni zetu kama KIBEBEO kutupa furaha; Mungu hutumia umasikini wetu kama kibebeo kutupa utajiri; Mungu hutumia udhaifu wetu kama kibebeo kutupa nguvu; Mungu hutumia ugonjwa wako ulionao kama kibebeo cha kukupa afya.

Daudi hakumshinda Goriath kwa nguvu zake, bali alimshinda kwa KIBEBEO alichokiona Goriathi kuwa ni kumdharau na kumkejeli kuwa hawezi. Mungu alitumia udhaifu huo huo kuonesha nguvu zake kwa Goriath. "...*Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu (1 Wakorintho 1:27)".* Udhaifu ni kibebeo cha kupewa nguvu, kudharauliwa ni kibebeo cha kupewa heshima. Yamkini upo kipindi kigumu, watu wanakucheka, wewe wambie Mungu ananitengenezea kibebeo cha baraka zangu nyingi zijazo. Japo nalia kwa sasa, lakini kilio changu ni kibebeo cha furaha yangu ya kesho. "*Wapandao kwa machozi Watavuna kwa kelele za furaha" (Zaburi 126:5)".*

Machozi ni kibebeo cha kelele za furaha. Angalia mstari unaofuata, ingawa mtu anakwenda zake akilia, achukuapo mbegu za kupanda. Hakika atarudi kwa kelele za furaha**,** aichukuapo miganda yake. Bado kibebeo cha kilio kinakuwa furaha. Swali, kibebeo chako ni kipi kwa sasa, ili unapoenda mbele za Mungu ajue ni nini? Yabesi alikuwa na huzuni na Mungu alitumia huzuni kama kibebeo cha kumpa furaha yake. Je, una kibebeo gani? Siyo kifungashio msomaji wanguu!! "Asomaye na afahamu".

## 6. Ukitaka Kufanikiwa Kimaisha Kubali Kwenda Kinyume na Mazoea

Historia ya Yabesi haikuwa nzuri ndio maana Yabesi aliamua kuomba Kwa uchungu na akakataa Mazoea. Hali ya wana wote wa Yuda jinsi walivyokuwa wakiishi; akina Huri,j amaa za Wathorathi, Naara, wana wa Simeoni, akaenda kinyume na walivyozoea. Kumbuka "**mazoea hujenga tabia**", kama umezoea kutoa Shilingi 500 kanisani hata kama atatokea mtu akakupa Shilingi 10,000, kwa sababu ya roho ya mazoea utatafuta chenchi maduka yote ili upate hiyo uliyozoea kutoa ambayo ni shilingi mia tano. Kumbuka **"Kiwango chako cha kumtolea Mungu kibadilike kutokana na vile unavyobarikiwa"** maana utoaji wako ndiyo unaoamua baraka zako. Umezoea mtaji wa mfuko mmoja wa sukari hata kama utapata faida ya mifuko mitatu bado utaleta mfuko mmoja hiyo ni roho ya mazoea inakutesa.

Wakoma hawakukubali hali waliyokuwa nayo, walienda kinyume na mazoea. Biblia inasema "*Basi walikuwapo watu wanne wenye ukoma, penye lango la mji; wakasemezana,* ***Mbona tunakaa hapa hata tufe?*** *Tukisema, Tutaingia mjini, mjini mna njaa, nasi tutakufa humo; nasi tukikaa hapa, tutakufa vile vile. Haya! Twende tukaliendee jeshi la Washami; wakituhifadhi hai tutaishi; wakituua, tutakufa tu". 2 Wafalme 7:3-2*0)".Wakoma wanne walikataa hali ya mazoea ya kukaa na njaa, walichukua hatua ya imani maana imani isiyokuwa na matendo imekufa, walipofanya hivyo walikula na kusaza chakula.

Yabesi hakukubali kufa na huzuni alijisemea moyoni, naenda kinyume na huzuni ikawe furaha haijalishi nilivyo leo; lakini Mungu anajua kesho yangu lazima niingie kwenye maombi ya kug'ang'ana na Mungu wangu. Ni sawa tu alichokifanya Danieli kwa Waamedi na Waajemi--walizoea kuroga roga. Kila mara Danieli alipoomba alibadili mazingira "*Hata Danieli, alipojua ya kuwa yale maandiko yamekwisha kutiwa sahihi, akaingia nyumbani mwake, na madirisha katika chumba chake yalikuwa yamefunguliwa kukabili Yerusalemu; akapiga magoti* ***mara tatu kila siku, akasali, akashukuru mbele za Mungu wake,*** *kama alivyokuwa akifanya tokea hapo (Danieli 6:10-15)".*

Danieli alienda kinyume na mazoea ya Waamedi na Waajemi ndipo inaleta matokeo chanya kwa mfalme, na mfalme anasema ule mstari wa 26 "*Mimi naweka amri, ya kwamba katika mamlaka yote ya ufalme wangu watu watetemeke na kuogopa mbele za Mungu wa Danieli; maana yeye ndiye Mungu aliye hai, adumuye milele, na ufalme wake ni ufalme usioharibika, na mamlaka yake itadumu hata mwisho*". Wakati

Shadraka, Meshaki na Abedinego wanakataa kuabudu sanamu ya mfalme Nebukadneza wale walioabudu maliwali walizoea kufanya hiyvo, lakini hawa Wakaldayo wakaenda kinyume na mazoea. Nini kilitokea kwa mfalme? Mfalme anasema "N*ebukadreza akanena, akasema, Na ahimidiwe Mungu wa Shadraka, na Meshaki, na Abednego; aliyemtuma malaika wake, akawaokoa watumishi wake waliomtumaini, wakaligeuza neno la mfalme, na kujitoa miili yao ili wasimtumikie mungu mwingine, wala kumwabudu, ila Mungu wao wenyew*e (Danieli 3:28)". Ooh! Haleluya! Ni Siri ya ajabu kweli hii ukifanya mambo bila mazoea Mungu hujifunua kwa namna isiyokuwa ya kawaida.

Petro na wenzake walizoea kuvua samaki wengi usiku lakini anakuja Bwana aliye kinyume Cha mazoea anabadili password cheki Petro anavyosema ...*"tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu; lakini kwa neno lako nitazishusha nyavu*". Walizoea usiku na usiku nao hawakupata lakini walipokubali kwenda kinyume na mazoea nini kilitokea? Walipata samaki wengi mno, nyavu zao zikaanza kukatika (Luka 5:6).

**"Mazoea ni adui mkubwa wa muujiza wako", ukizoea kufanya mambo yale yale siku zote utapata matokeo yale yale uliyozoea.**

Lakini ukifanya tofauti utapata matokeo tofauti pia. Ukiomba kwa mazoea utapata kwa mazoea pia. Kama umezoea kuomba dakika kumi mwaka huu acha mazoea ongeza dakika angalau ziwe kumi na tano na kama ulikuwa unaomba saa moja, nenda saa moja na nusu. Kataa mazoea ili ufanikiwe kiroho na kimwili pia. Je, umezoea kufanya nini kanisani? Je, umezoea kuomba dakika ngapi? Je, kanisani kwenu mmezoea kitu gani na hamwoni mnafanikiwa? Je, kitu kipi kinakurudisha nyuma? Na kama ndiyo, hicho ndicho umezoea?

## 7. "Yabesi Akamlingana Mungu wa Israeli"

*"...Huyo Yabesi akamlingana Mungu wa Israeli... (1 Mambo ya Nyakati 4:10)".* **"Kumlingana",** ni Kiswahili cha zamani kilichotumika kikiwa na maana ya kuomboleza kwa kuomba, kumlilia Mungu kwa kuomba, au kumwomba Mungu. Ni sawa na kusema Kiswahili cha neno 'Kumlingana' ni kumlilia, au neno lenye maana sawa na kumlingana ni kumlilia. Hivyo Yabesi aliomba Mungu wake kibinafsi kama mtu aliyekwama kimaisha.

Kumbuka maombi ni kama 'bomu la kiroho' (Spiritual atomic bomb), likirushwa lazima liangamize. Pia maombi ni vita, maombi ni mawasiliano kati Mungu na mwumini au miungu, na mawasiliano haya ndani yake yaana mkono wa kupokea majibu kutoka

kwa Mungu unaoitwa Imani, na imani chanzo chake ni kusikia Neno la Kristo " *Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo (Warumi 10:17)".* Kwa hiyo maombi lazima yawe na imani ndani yake. Maombi ni furushi (package) iliyobeba ndani yake imani na Neno la Mungu, sawa! Ngoja nikupe formula ya maombi:

**Imani + Neno la Mungu = Maombi.**

**Imani** ndiyo mkono wa kupokea kitu kutoka Kwa Mungu uliobeba mambo yajayo na bayana (waziwazi) ya mambo yasiyoonekana. Sasa yanaonekana kama yasiyokuwako kana kwamba yamekuwako na Neno la Mungu ni uthibitisho wa kile alichokisema Mungu kwa tafasiri nyingine ni marejeleo (references).

Kumbuka anasema "...*ninaliangalia neno langu, ili nilitimize (Yeremia 1:12)*". "*Ndivyo litakavyokuwa neno langu, litokalo katika kinywa changu; halitanirudia bure, bali litatimiza mapenzi yangu, nalo litafanikiwa katika mambo yaleniliyolituma( Isaya 55:11)*".

## SURA YA PILI

### Sayansi ya Maombi ya Yabesi

Maombi ni sayansi iliyo na mlinganyo sawia uliobeba ndani yake Neno la Mungu. Neno la Mungu ni 'busta' inayosukuma maombi haraka. Ninaposema busta kwa wale wakulima wa mazao wanajua busta ina kazi ya kuyasukuma mazao yaliyodhoofika ili yakue haraka, ndivyo ilivyo kwa Neno la Mungu!

Sayansi ya maombi ya Yabesi ilikuwa inaonesha **Kuomba, Mpaka, Kitu, Kitokee** yaani kwa Kiingereza tunaita '**PUSH'.**

**P = Pray**

**U = Until**

**S = Something**

**H = Happen**

Kwa Yabesi mpaka kilitokea alichokitaka ndiyo maana Biblia inasema alipomaliza kumlingana Mungu wa israel... "*Naye Mungu akamjalia hayo aliyoyaomba (1 Mambo ya Nyakati 4:10) ".* Aling'ang'ana kama Yakobo aliyeteguliwa paja na Penieli alishindana naye, tunaita **maombi ya kushindana.**

**Yabesi aliomba kwa Mungu anayemjua;** siyo Kwa Mungu asiyejulikana kama Mungu wa Efeso Artemi au Diana aliyeyumbisha imani za watu wengi mpaka Paulo anamwandikia Timotheo mwanae wa kiroho juu ya kanisa la Efeso kuwa macho ya mioyo yenu yatiwe nuru dhidi ya roho zidanganyazo "*macho ya mioyo yenu yatiwe nuru... (Waefeso 1:18)".*

**Yabesi aliomba kwa Mungu anayemjua vyema;** na akaainisha ni Mungu yupi wa Israeli. Kumbuka huyu Yabesi anajua vyema kuwa huyu Mungu wa Israeli siyo feki ni origino na anajua matendo yake makuu aliyoyafanya alivyowavusha wana wa Israeli Bahari ya Shamu; aliyesimamisha Jua wakati wa Joshua; aliyeinua Nyoka wa Shaba

kule Misri; aliyewaua miungu ya baali wakati wa Eliya. Ndiyo maana anaomba kwa Mungu wa Israel. Je, wewe unaomba kwa Mungu yupi? Sawa wewe ni mkristo sikatai, ila Mungu wako ni yupi? Ndiyo unaimba kwaya sijakataa, je Mungu wako ni yupi? Mashetani nao wanaamini Mungu ni wao kama wewe. Yakobo anasema "*Wewe waamini ya kuwa Mungu ni mmoja; watenda vema. Mashetani nao waamini na kutetemeka (Yakobo 2:19 )".*

**Nyakati za agano la kale kulikuwa na miungu mingi sana**; lakini aliyekuwa kiboko wa wote ni Mungu wa Israeli ndiyo maana kulipotokea ubishi wa kidini kati ya Eliya na miungu ya baali, Eliya aliomba Kwa Mungu wa Israeli. Anasema *"Na ijulikane leo ya kuwa wewe ndiwe Mungu* **katika Israeli, na ya kuwa** *mimi ni mtumishi wako, na ya kuwa nimefanya mambo haya yote kwa neno lako (1 Wafalme 18:36)*." Alipomaliza kuomba tu moto ulishuka na Mungu wa Israeli akajibu kwa moto.

Swali langu ni hili; Yabesi kwanini aliomba kwa Mungu wa Israeli? Japo kulikuwa na miungu mingi tu iliyotoa majibu kipindi hicho? Kama mungu wa baali, mungu wa Ashera, mungu wa Ekroni na Mungu wa Dagoni? Kwa nini hakuomba wa hiyo miungu?

Nakumbuka nilikuwa nahudumia mkutano wa Mtoto wa Rehnald Bhonke mwaka 2012 katika viwanja vya Furahisha kama mhudumu (usher), tukiwa kwenye mkutano mhubiri alisema jambo ambalo mpaka leo sisahau. Alisema mbele ya waliopita kuokoka akasema ("I**f we pray to God, we should pray to a known God but not to unknown God").** Yaani alimaanisha "k**ama tukiomba lazima tuonamba kwa Mungu tunayemjua lakini siyo Mungu tusiyemjua**". Akaanza kuomba alipomtaja tu Mungu wa Israeli, pale pale tuliona matendo makuu ya Mungu. Nilikuwa nimesimama karibu na mama hatembei nilimwona mama huyo anatembea pale pale! Hii ndiyo sababu Yabesi alijibiwa maana aliomba kwa Mungu aliye na uhakika naye.

## 8. Yabesi Alikuwa Mtu wa Kawaida Miongoni mwa Watu wa Kawaida

Yabesi alikuwa mtu wa kawaida, lakini baada ya kuomba maombi akawa mtu asiye wa kawaida miongoni mwa watu wa kawaida (extraordinary person among the ordinary people). Maombi yalibadilisha ukawaida wake na kuwa mtu asiye wa kawaida. Haujawahi kusikia mtu anasema, mimi ni mkristo wa kawaida, akimaanisha kuna vitu havifanyi kama mkristo, wewe siyo mkristo wa kawaida. Baada ya maombi ya Yabesi kuna mambo yalitokea kwake:

(i). Anwani ya Yabesi ilibadilika, badala ya sanduku la posta huzuni likawa sanduku la postal furaha

(ii). UKawaida wake ukawa mtu asiye wa kawaida

(iii). Laana ikawa baraka (nibariki kweli kweli)

(iv). Mipaka iliyofungwa baada ya maombi ikapanuliwa

(v). Alikuwa mawindo ya shetani baada ya maombi akalindwa dhidi ya uovu

(vi). Shetani alimteka maisha yake yote baada ya maombi mkono wa Bwana ukawa pamoja naye

Hii ndiyo sababu alikuwa mtu wa kawaida miongoni mwa watu wa kawaida. Baada ya maombi mambo akabadilika akawa mtu asiye wa kawaida miongoni mwa watu wa kawaida. Biblia imezungumzia 'mnyonge' kama mtu wa kawaida "*Humwinua* ***mnyonge*** *kutoka mavumbini (1 Samweli 2:8)".*

Ngoja nikupe ushuhuda kidogo; wakati nipo sekondari, kuna mwalimu alikuwa anatusumbua sana na hasa wakati wa kipindi cha dini, alikuwa akipita anagonga milango vikundi vyote vya dini pale shuleni kisa muda umeisha wa ibada, hata kama muda haujaisha, na tulikuwa waaminifu sana kwenye muda ili tusivunje sheria za shule. Yule mwalimu alitukera sana tukawa tunamwombea tu Mungu amsamehe.

Siku Moja akiwa anafundisha binti mmoja akapagawa mapepo darasani, akaanza kuwatwanga ngumi wanafunzi wenzake huko mbele ya darasa. Mwalimu alipoona hivyo naye akaanza kurusha ngumi. Cha ajabu yule binti alimtwangwa mwalimu ngumi moja mpaka chini. Binti yule akambana yule mwalimu hapo chini huku akimpiga gumi. Yule binti alijigamba darasa zima na mwalimu hakupata msaada. Ghafla mimi nikiwa nyuma nilisukumwa kwenda kumtoa yule mwalimu huku nikikemea huyo pepo. Nakumbuka nilisema, kwa jina la Yesu mwachie mwalimu wetu.

Nilirudia kama mara tatu kisha yule binti akaanguka chini na yule mwalimu akaondoka. Nilianza kumwombea yule binti kisha kwa neema ya Mungu akawa huru. Kuanzia siku hiyo, huyo mwalimu aliheshimu sana vipindi vya dini. Tukawa tunasikia waalimu wakiongea ofisini, hao watu siyo wa kawaida kumbe!! Kumbe tulionekana wa kawaida miongoni mwa watu wa kawaida, kumbe sisi siyo wa kawaida miongoni mwa watu wa kawaida.

Daudi alionekana mtu wa kawaida katika kambi ya waisraeli, ndiyo maana walimvika mavazi ya kivita ili apigane na Goriath, lakini aliyakataa maana alijua siyo mtu wa

kawaida miongoni mwa watu wa kawaida; alijua ana nguvu kuliko anavyoonekana. Kibinadamu Goriath alionekana ana nguvu lakini kumbe Daudi alikuwa na nguvu ndiyo maana Daudi anasema, ili kuonesha mimi siyo wa kawaida anasema "*Daudi akamwambia Sauli, Asizimie moyo mtu ye yote kwa ajili ya huyu; mimi mtumishi wako nitakwenda kupigana na Mfilisti huyu (1 Samweli17:32)".* Hii ni lugha ya mtu asiye wa kawaida.Y abesi alipojitambua kuwa yeye siyo wa kawaida katika wana wa Yuda ndiyo maana alijikubali na akamlingana Mungu wa Israeli.

## 9. Unyenyekevu wa Yabesi Ulitengeneza Maombi Binafsi ya Kimkakati

Pamoja na kuheshimiwa Yabesi na nduguze, lakini bado alinyenyekea na kwenda mbele za Mungu na agenda zake tano (5) za kimkakati. Hebu fikiri mtu na heshima zake ananyenyekea mbele za Mungu kwa maombi. "...*nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake (1 Petro 5:6)"* .Kanuni ya kuinuliwa ni kunyenyekea .

Yabesi alijishusha na akaingia kuomba maombi binafsi ya kimkakati na alimwamini Mungu wake na Mungu alimjibu. Ile kwamba wewe ni mbunge nyenyekea tu, ile kwamba wewe ni mwimbaji jifunze kunyenyekea, Mungu akikuinua, hakuna mwanadamu atakayekushusha chini. Lakini mwanadamu akikuinua ni rahisi sana kukushusha chini. Usitafute umaarufu na 'usupastaa' kanisani, bali utafute uso wa Mungu kwa njia ya 'Maombi Binafsi ya Kimkakati' kama Yabesi.

**Maombi ya Yabesi hayakuwa ya kitaifa au ya kifamilia isipokuwa yalikuwa maombi binafsi ya kimkakati;** nampenda Yabesi maana alisimama yeye kama yeye akaelezea mambo yake yoote *"Unikumbushe, na tuhojiane; eleza mambo yako, upate kupewa haki yako (Isaya 43:26)*". Si kila tatizo linalokusumbua umwambie kila mtu, kuna mambo ambayo ni nyeti hata ni aibu kumwambia mtu ila Mungu ukimwambia kwa njia ya maombi atakusikia.

**Maombi ya Yabesi yanatengeneza waombaji na siyo waombewaji;** ndiyo maana ukipona wewe katika kuomba kibinafsi kwanza utaweza kuombea familia, ukiombea familia, kisha utaombea kanisa, ukiombea kanisa msukumo utakaokuja ni kuombea taifa.

**Kanisa la leo lina waumini wengi waombewaji na siyo waombaj**i; hapa usinielewe vibaya kwamba napinga kuombewa, ninachotaka kila mtu aweze kujipigania yeye kama yeye mpaka anavuka, hata ikitokea Askofu au Mchungaji wako hayupo.

Utaombewa mpaka uote kipara jamani! Ndiyo maana wanafunzi wa Yesu walifika hatua wakachoka kuombewa ikabidi wamwambie Yesu kwamba, "...*wanafunzi wake alimwambia, Bwana, tufundishe sisi kuomba (Luka 11:1)*".

**"Bora usimpe mtu samaki, bali mfundishe mtu jinsi ya kuvua samaki";** ndiyo maana leo kwa sababu ya uvivu wa kutokuomba, shetani amebuni njia mbadala wa maombi, ndiyo maana leo kuna vifaa vya upako wanaita chumvi, maji, kokoto, mafuta, viboko, keki, asali, matunda na kila aina ya uchafu. Lakini swali la kujiuliza, je umeshindwa kuomba kama Yabesi? Hebu na wewe fuatilia hao wanaotumia hivyo vitu angalia hali zao za kiroho je, wamesimama? Au kiroho chao kimepotea? Fanya utafiti na wewe! Ukiwasimamisha kujielezea kuhusu Neno la Mungu ni wabishi tu hata ile nguvu ya kuomba haipo tena. "*Na manabii wengi wa uongo watatokea, na kudanganya wengi. Na kwa sababu ya kuongezeka maasi, upendo wa wengi utapoa (Mathayo 24:11-15)*". Lakini mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakayeokoka.

Katika Agano la Kale kulikuwa na manabii wengi sana wenye upako na kulikuwa na manabii wakubwa kwa wadogo lakini je, kwanini Yabesi hajaenda kwa hao manabii kupeleka shida zake kama wengine walivyofanya? Kama yule Namani, jemedari wa jeshi la mfalme wa Shamu aliyeenda kwa Elisha kuuliza kupona ukoma? Kumbuka kulikuwa na Samweli, Eliya na manabii wengine. Kwa nini huyu Yabesi aling'ang'ania yeye tu kuomba binafsi? Kwa nini asiende huko kwa akina Eliya, Samweli na wengine? Aliamini akiomba yeye atasikiwa.

Kwanza kumbuka "**Si Kila anayekuzunguka anakupenda",** yamkini hata kukuombea hakuombei japo atasema mtumishi nakuombea kumbe hata hakuombei ila anauchapa usingizi usiku kucha. Bora ukaombe wewe kama wewe unayejua shida yako na uzito wa mzigo wako. Yabesi aliamua kuomba binafsi ili mambo yake yafufuke japo alionekana hai ila alikuwa amekufa kiroho kama vile Yohana alivyowaandikia watu wa Sardi katika kitabu cha Ufunuo wa Yohana, "*Haya ndiyo anenayo, Nayajua matendo yako, ya kuwa una jina la kuwa hai, nawe umekufa. (Ufunuo 3:1)".*

**Nidhamu ya maombi ya Yabesi ilitokana na Moyo wa unyenyekevu;** moyo uliopondeka wa kuomba mbele za Mungu kimkakati. Ninaposema kimkakati ndani yake kuna kuwa na agenda muhimu zilizobeba kusudi maalumu juu ya maombi hayo. Unyenyekevu wako ukoje uwapo kanisani? Je, wakati unaomba huwa unachati na simu? Au hutulii kanisani mara nje mara ndani utafikiri unauza mayai au karanga? Je, unyenyekevu wako kwa Bwana juu ya utumishi wako ukoje? Au unajigamba kwamba hapa kanisani mimi ndiye mimi hamna mwingine; yaani kwa lugha nyingine wewe ni kama jenereta la kanisa usipokuwapo hamna kitakachofanyika, je uko hivyo? Au ile

kwamba mapepo yanakutii unaombea tu mara moja mtu anafunguliwa basi hata mchungaji hakohoi. Je, uko hivyo?

Kumbuka "**Kiwango chako cha unyenyekevu na maadili katika huduma yako ndicho kitakachoamua umbali wa safari ya huduma yako"** hautafika mbali. Wewe unayeimba, unayehudumu, unayehubiri kama hutanyenyekea; maana kilichomfanya shetani apigwe ni kiburi kutaka kusifiwa na kuabudiwa. Mtumishi yeyote wa Mungu ni punda aliyembeba Yesu, siku Yesu akishuka watakuponda mawe. Jifunze kunyenyekea maana shetani haogopi Padri, Nabii, Mzee wa kanisa, Mchungaji na vyeo vyote unavyovijua. Shetani anaogopa mwombaji mnyenyekevu. Mtumishi yeyote lazima awe na kitendea kazi muhimu kiitwacho **Maombi,** maana maombi ni harufu mbaya kwa shetani na manukato mazuri kwa Mungu "...*manukato, ambayo ni maombi ya watakatifu. (Ufunuo 5:8)".*

## 10. ”Lau kwamba Ungenibariki Kweli kweli”

"...*Lau kwamba ungenibarikia kweli kweli (1 Mambo ya Nyakati 4:10 )".* Neno"**Lau"** linamanisha ulinganifu wa vitu au kitu kwa kiswahili sanifu lakini. Kwa tafasiri ya Kibiblia linamaanisha ni kitendo cha kuongea kwa hisia kutoka ndani kunakoonesha kwamba unaumia au kufurahia kibinafsi (person emotional). Mfano, mtu anapata tatizo furani ili kuonesha mguso furani wa ndani utasikia anasema Ashiiiiii!! Uwiiii!! Ayiiii!! Mamaaaa!! Ohooooh! Woohoo!! Badala ya kusema hayo maneno Yabesi anasema "**LAU"**, kuonesha kuumia sana na kuguswa ni sawa na Yesu alipokuwa Msalabani alionesha kuumia kwa kusema "...***Eloi, Eloi,*** *lama sabakthani? Maana yake,* ***Mungu wangu, Mungu wangu,*** *mbona umeniacha?* (Marko 15:34)".

Kati ya mambo muhimu mojawapo aliyoomba Yabesi ni kubarikiwa kweli kweli siyo kubarikiwa tu. Kuna utofauti wa mtu kusema vizuri na vizuri sana. Sasa Yabesi anaomba abarikiwe kweli kweli siyo tu kubarikiwa, bali kubarikiwa kweli kweli. Maana yake apate upendeleo wa kiMungu, kama alimwomba Mungu amubariki, uwe na hakika baraka za Mungu zilikuja na furaha. Kumbuka baraka za kishetani zina masharti yanayokufanya uwe mtumwa usiye na amani, mwenye huzuni siku zote lakini baraka za Mungu, *"Baraka ya BWANA* ***hutajirisha****, Wala hachanganyi* ***huzuni n****ayo(Mithali 10:22)".*

Kama Yabesi alibarikiwa kwa kuomba baraka, uwe na uhakika aliomba na ulinzi pia. Kumbuka" **ukiomba Mungu akubariki usisahau kuomba na ulinzi pia",** yaani Mungu akulinde. Unazikumbuka zile baraka za Haruni anasemaje? "*BWANA akubarikie, na* ***kukulinda (Hesabu 6:24*****)".** Ukishabarikiwa unahitaji ulinzi. Kuna baraka na

mafanikio na utajiri. Mafanikio yanaanzia rohoni yanayokufanya uishi katika kusudi la Mungu. Unaweza kuwa huna hela lakini umefanikiwa, una amani, furaha na upendo, ndiyo maana ya mafanikio, maana furaha haitokani na pesa. Utajiri siyo baraka, unaweza ukawa tajiri lakini bado laana inakutafuna. Baraka imebeba kila kitu; Paulo aliwahi kusema katika Waefeso 1:3, Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ***aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo.***

Tanzania tuna ruzuku mbalimbali mfano ruzuku ya mbolea ruzuku ya pembejeo n.k, maana yake kama ulitakiwa kununua mbolea mfuko wa NPK 70,000/= watakuuzia 20,000/= Pesa inayobaki serikali inakulipia. Sasa nisikilize, ruzuku ya Mungu kwetu sisi ni baraka; tunapataje baraka? Kwa kufanya kazi "**Mahali pekee pa Mungu kupitishia baraka zake ni kazi".** Yabesi aliomba baraka uwe na uhakika alikuwa na kazi ya kufanya. Biblia inasema alikuwa na kiwanja japo kilidumaa ndiyo maana anasema panua hozi (mipaka). Maana yake, huwezi kuomba mpaka ukue kama huna mpaka. Kwa hiyo kuna kazi alifanya kwenye umiliki wake (territory) maana **"Baraka za Mungu kuja kwa mwanadamu zimefichwa ndani ya kaz**i". Maana kazi ni baraka kutoka kwa Mungu na siyo laana, hivyo fanya kazi kwa bidii. Ruzuku yetu kutoka Kwa Mungu ni baraka, upendeleo mwingine utakaouona ni pale unapofanya kazi maana **"kazi ni uhai".** Kila mtu amekuja duniani na kazi--hakuja na ajira, hivyo kazi ni nyingi ajira ni chache. Mungu anasema, atakufunulia BWANA hazina yake nzuri, nayo ni mbingu, kwa kutoa mvua ya nchi yako kwa wakati wake, **na kwa kubarikia kazi yote ya mkono wako**; nawe utakopesha mataifa mengi, wala hutakopa wewe na atabariki tena kazi ya mikono iliyo halali.

**Ukibarikiwa na wewe ujikubali**; Yabesi hakujikatia tamaa pamoja na kuwa na huzuni alijikubali yeye anaweza. Mariamu alijikubali kuwa amebarikiwa kuliko wanawake wote! Na wewe jikubali jisemee kwamba wewe ni mzuri, jibariki mwenyewe! Jitamkie baraka maana uzima na mauti viko kinywani mwako! Usijilaani kuwa wewe mbaya hata ukijiona kwenye kioo unajisemea duh!! Uso wangu wa mbuzi! Ona sina hata miguu, nina milonjo tu jamani! Ona shepu yenyewe haipo kama ubao! Jitamkie mema kuwa wewe ni shujaa kama Gideoni. Gideoni alijidharau lakini malaika akamwambia yeye ni shujaa laweza neno jema kutoka kwako amini mpendwa, Ooooh Haleluya! Kanuni ya kubarikiwa (kuongezeka) inasema hivi, *"Bali utafuteni kwanza ufalme... mtazidishiwa (Mathayo 6:33)".*

## 11. Mungu Haangalii Umeanzaje, Anaangalia Unamalizaje

Maombi ya Yabesi yalileta uamusho uliobadili mwanzo mbaya na kuwa mwisho mwema "*Heri mwisho wa neno kuliko mwanzo wake (Mhubiri 7:8)".* Usijikatie tamaa jinsi ulivyo, Mungu anakupa leo nafasi ya pili kama ile aliyopewa Yona. Yuda alianza vizuri akamaliza vibaya kwa kujinyonga! Sauli ambaye ni Paulo alianza vibaya kwa kulitesa Kanisa akamaliza vizuri kwa kuhubiri injili Asia yote; Rahabu yule kahaba alianza vibaya akamaliza kwa kuwapokea wale wapelelezi!

Najua umeanza vibaya kwa kutoa mimba, kufanya uasherati na uzinzi; mwaka umeanza vibaya kwa misiba; omba kama Yabesi ili unapomaliza mwaka huu umalize vizuri. Fikiria shetani amekula afya na sasa ni mgonjwa, amekula ndoa huna amani na yaliyosazwa na ugonjwa yameliwa. Nabii Yoeli anasema "y*aliyosazwa na tunutu yameliwa na nzige; na yaliyosazwa na nzige yameliwa na parare; na yaliyosazwa na parare yameliwa na madumadu (Yoeli 1:4* )". Umeanza Kwa kushambuliwa hata kile kinachobaki kikusaidie, bado nacho kinaliwa na nzige na madumadu. Ikiwa umeanza vibaya kwa kushambuliwa, Mungu anasema leo kwako mwaka huu ni **urejesho--a**nasema hayo yote yaliyoliwa na yakasazwa anasema, *"Nami nitawarudishia hiyo miaka iliyoliwa na nzige, na parare, na madumadu, na tunutu, jeshi langu kubwa nililotuma kati yenu. (Yoeli 2:25)".*

Yabesi alianza kwa akili zake mwenyewe, lakini ilifika mahali akili zikafika mwisho ikabidi amtumaini Mungu wa Israeli "*Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe (Mithali 3:5)".*

## 12. Yabesi Hakuomba Maombi ya Kulalamika, Lakini Nabii Habakuki Aliomba Maombi ya Kulalamika

Maombi ni kukaa kikao na Mungu na kikao chochote lazima kiwe na agenda muhimu na zenye mashiko. Yabesi hakwenda mbele za Mungu kwa kuanza kulalamika, alienda moja kwa moja kwenye ajenda na ajenda zake zilikuwa kama zifuatazo:

(i). Kukataa huzuni ya muda mrefu

(ii). Kuzidisha hozi (mipaka)

(iii). Ungelinda na uovu

(iv). Bwana ungenibariki kweli kweli

(v). Mkono wa Mungu uwe pamoja nami

Huwezi kwenda mbele za Mungu bila agenda, na alipoanza kuombea hizo agenda, Mungu alimjalia yale aliyoyaomba. Hii inaonesha ni wa jinsi gani Yabesi alikuwa na mzigo wa kuomba kibinafsi. Unapokuwa na mzigo wa kuombea jambo fulani, Mungu atakupa siri nyingi juu ya hicho unachokiombea. Mfano, ukiombea Kanisa Mungu atakupa siri nyingi juu ya Kanisa; vilevile katika mambo ya kifamilia au nchi. Mungu hawezi kukupa siri juu ya jambo ambalo huna mzigo nalo--atawafunuliwa walio na mzigo, "*Hakika Bwana MUNGU hatafanya neno lo lote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake (Amosi 3:7)".*

Habakuki ni moja wapo wa manabii kumi na wawili (12), yeye kama nabii mdogo aliyepata nafasi ya kuomba, ilipofika zamu yake ya kuomba hakuomba sawa sawa, badala yake akaanza kulalamika. Embu angalia maombi yake ya kulalamika katika Habakuki 1:2-4:

(i). Ee BWANA, nilie hata lini, wewe usitake kusikia? (b) Nakulilia kwa sababu ya udhalimu, ila hutaki kuokoa

(ii). Mbona wanionyesha uovu, na kunitazamisha ukaidi?

(iii). Kwa maana watu wabaya huwazunguka wenye haki; kwa sababu hiyo hukumu ikipatikana imepotoka

Huyu nabii hana agenda zenye mashiko. Kumbuka tofauti na Yabesi wakati huo Habakuki aliliandikia kanisa la Yuda kipindi hicho limegawanyika, Yuda na Benyamini walipochukuliwa kwenda Babeli miaka 625. Habakuki anaona katika nchi yake hakuna haki hata kama ikipatikana imepotoka, rushwa imekithiri, uonevu mwingi, nchi hiyo watu wanatumia madaraka yao vibaya, ilipofika zamu yake ya kuomba juu ya hayo maovu alilalamika.

**Ukiomba kwa kulalamika Mungu atakujibu kulalamika kwako**". Habakuki inabidi aingie gharama ya kuomba tena mara ya pili ya kusimama katika zamu yake ya kuomba "*Mimi nitasimama katika* ***zamu yangu,*** *nitajiweka juu ya mnara, nitaangalia ili nione atakaloniambia, na jinsi nitakavyojibu katika habari ya* ***kulalamika kwangu (Habakuki 2:1)".***

## 13. "Kunizidishia Hozi Yangu"

"***...****kunizidishia hozi yangu... (1 Mambo ya Nyakati 4:10*). "Hozi" ni mipaka. Wakati wa Joshua watu walitakiwa kumiliki na kuongezeka; anaposema kunizidishia hozi yangu maana yake ni kupanua ardhi yenye mipaka halali ya kiumiliki. Maana nyingine

kupanua mtaji; ndiyo maana katika kila nyanja ya maisha yako unahitaji kuongezeka na siyo kudumaa! Kama ni kiwanja ukijenge kama ni kanisa lipanuke, kama ni elimu iongezeke kutoka ngazi ya cheti mpaka shahada na kutoka shahada mpaka shahada ya uzamivu. Aliye kidato cha pili aingie cha tatu; aliye cha nne aingie cha tano; aliye cha sita aende Chuo Kikuu; huku ndiko kupanuka. Nabii isaya akasema *"Panua mahali pa hema yako, na wayatandaze mapazia ya maskani yako; usiwakataze; ongeza urefu wa kamba zako; vikaze vigingi vya hema yako (Isaya 54:2)"*. Kama unauza nyanya uanze kuuza nguo upanuke/ukue kiuchumi, kitaaluma, kisiasa, kihuduma na kibiashara katika jina la Yesu; maana tunatoka utukufu hadi utukufu, neema hadi neema, kibali hadi kibali. Kwa maana ndani yake Yeye tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu.

Mipaka ya Yabesi ilifungwa lakini ashukuriwe Jehova El-Gibbo aliyefanya miujiza ya kumjibu huyu mwanaume Yabesi, japo aliona kama amechelewa lakini ahadi za Mungu ni za kweli. Wako watu wanapanga mipango na haipangiki na bado wanapenda kutafuta majibu kwa miungu mingine na hawapati majibu. Omba maombi ya Kiyabesi yaliyoleta matokeo chanya kwake na kwa kizazi chake. Usipange mipango ukaishia kuongea tu; unapata mshahara au unafanya kazi hata huoni unachofanya, ujue mipaka yako imefungwa! Yaani kwenye ulimwengu wa roho shetani amekuchorea mstari kwamba huwezi kuvuka. Jifunze tu kuomba kwa kupambana wewe kama wewe.

Omba kama Yabesi, yaani mnatamani nyumbani kwenu muolewe lakini mnaishia kuzalia nyumbani, ujue umechorewa mstari wa kichawi; umesoma sana umekomea kidato cha nne, ujue umechorewa mstari wa kichawi; umepata sana hela mwisho ni kushika milioni moja, au laki moja au elfu hamsini--yaani hauvuki hapo, ujue umewekewa mipaka ya mistari ya kichawi. Yabesi alichorewa mstari wa kutokupanuka na ndiyo maana akasema, panua hozi yangu.

Ndiyo maana huvuki japo unafanya kazi, Neno la Mungu linasema "*Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu (Wafilipi 4:6)".* Ni kuomba tu kama Yabesi anaposema na haja zenu anamaanisha agenda zenu kama zile za Yabesi! Je, agenda zako ni zipi? Zitaje sasa na uanze kuziombea.

**UKIRI: Ee Mungu nirehemu mimi (taja jina lako) nitakase kwa damu ya mwanakondoo; naomba upanue mahali pa hema yangu; mahali pa kazi zangu kwa jina la Yesu. Natangaza kuanzia leo, hiyo mipaka iliyofungwa nisisogee naiondoa kwa Jina la Yesu, roho ya chuma ulete achia, uchawi wa kuchora mistari teketea kwa Jina la Yesu naikomboa familia yangu na kuifunika kwa damu ya mwanakondoo. Amina!**

## 14. Mwombaji ni Chombo cha Dola ya Mbinguni

Mwombaji ni mlinzi katika ulimwengu wa roho ikumbukwe Kuna walinzi wa aina nyingi Kuna mgambo,makomanda,wanajeshi na polisi pia, waombaji nao ni walinzi wengine ni mgambo,wengine ni wanajeshi,wengine ni makomando Kwa hiyo tunatofautiana.uwe mlinzi yeyote Kwa maana ya mwombaji rungu lako ni Yesu Yeye ni Rungu kama yeye ni rungu na wewe ni rungu " *Wewe u rungu langu na silaha zangu za vita; kwa wewe nitawavunja-vunja mataifa; na kwa wewe nitaharibu falme (Yeremia 51:20 )*".

Mungu aliweka walinzi (waombaji) kule Yerusalemu" *Nimeweka walinzi juu ya kuta zako, Ee Yerusalemu; hawatanyamaza mchana wala usiku; ninyi wenye kumkumbusha BWANA, msiwe na kimya (Isaya 62:6)*". Je unajua wewe ni mlinzi? Yabesi alijua akiomba maombi ya kikuhani atatawala na kumiliki malango ya adui. Fikria Trafiki ni DOLA ya nchi, hata kama ni mdogo namna gani bado madereva watamheshimu vivyo hivyo. Hata wewe ni DOLA ya serikali ya mbinguni, awe mchawi au majini au mizimu lazima watii kutokana na mamlaka uliyopewa na mamlaka ya serikali ya mbinguni. Ndiyo maana Yesu anawambia wanafunzi wake katika, *Luka 10:19, Tazama, nimewapa* ***amri*** *ya kukanyaga* ***nyoka (shetani)*** *na* ***nge (uchungu)*** *na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru.*

Mwombaji yeyote yule ni chombo cha DOLA ya mbinguni una uwezo wa kufunga vitu pingu kwenye ulimwengu wa roho kama ikiwa ni viti vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka falme na mamlaka ya wakuu wa giza, majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho, na utakayoyafunga duniani yatakuwa yamefungwa mbinguni. Je, Yabesi alijua hivyo? Je, wewe unajua hivyo? Yabesi alijua hivyo ndiyo maana aliomba, japo aliheshimiwa kwa vyeo vyake, lakini aliendа kuwa mojawapo wa vyombo vya DOLA ya mbinguni kwa njia ya maombi!! Ooooh Haleluya!!!

## 15. "Mkono Wako Ungekuwa Pamoja Nami"

"*...mkono wako ungekuwa pamoja (1 Mambo ya Nyakati 4:10)*". Anamaanisha upendeleo wa kiMungu, kibali (Spiritual Favour). Yabesi pamoja na kuheshimiwa sana lakini hakuwa na upendeleo, hakuwa na upenyo ilibidi atafute mkono wa Mungu (uwepo wa Mungu). Mkono wa Mungu ukiwa pamoja nawe hauhitaji vyeti ili kutafuta kazi ,wao watakutafuta! Mkono wa Mungu ukiwa pamoja nawe hauhitaji kujitangaza kwenye vyombo vya habari ili utangaze huduma yako, wao watakutafuta. Maana ni

sauti ya mtu aliye nyikani! Mkono wa Mungu ukiwa pamoja nawe haihitaji utongoze kwanza ili uoe mbali. Mungu atakuletea aliye chaguo lako.

Mkono wa Mungu ukiwa pamoja nawe kuna vitu utapata bila kujua umepataje! Yaani unapofanya kazi yoyote watu waseme huu ni mkono wa Mungu, kiasi kwamba wengine wataenda mbali zaidi na kuanza kumtukuza shetani badala ya Mungu. Utasikia wanasema anatumia uchawi!, ni freemason! Ukisikia hivyo wambie huu siyo mkono wa mwanadamu ni mkono wa Mungu uko pamoja nami. Maana si kwa uwezo wako, wala si kwa nguvu zangu, bali ni kwa uwezo wa wa Mungu kupitia mkono wake.

Yabesi alipoomba mkono wa Mungu uwe pamoja naye, Mungu alimwinua sana. Kumbuka Mungu wetu humwinua mnyonge kutoka mavumbini, humpandisha mhitaji kutoka njaani ili awaketishe pamoja na wakuu. Yabesi Mungu alimwinua kuliko alivyotarajia. Jifunze kuomba mkono wa Mungu uwe pamoja nawe wala huhitaji kujipitisha pitisha kwa wanaume au wanawake wakuone ili wakuoe au uoe. Kama mkono wa Mungu upo pamoja nawe watajileta wenyewe yaani. Unakuwa na kibali, ukiwa na kibali kupitia hiyo biashara yako utafanya mambo makubwa maana, kila jambo ukiliweka mkononi mwa Mungu hakuna mtu wa kulipokonya.

Mkono wa Mungu ulikuwa kwa Danieli ndani ya tundu la Simba, mkono wa Mungu ulikuwa kwa akina Shadrack, Meshack na Abedinego ndani ya tanuru la moto. Mkono wa Mungu ulikuwa pamoja na wana wa Israeli jangwani na ndani ya Bahari ya shamu. Mahali ambapo akili ya mwanadamu inakomea ndipo hapo mkono wa Mungu unaaza kufanya kazi, maana..." a*kili zake hazichunguziki. (Isaya 40:28)".*

**UKIRI: Ee Mungu wangu nisamehe kwa kufanya mambo bila kuomba mkono wako uniongoze! Kuanzia leo rimoti ya kishetani inayoendesha maisha yangu naivunja kwa damu ya Yesu. Mikono ya kichawi iliyoshikilia hatima yangu vunjika kwa jina Yesu! Mahali niliposhikiliwa kwenye giza natoka huko kwa nguvu ya damu ya Yesu. Mkono wako uwe pamoja nami kuanzia leo nafunika roho yangu, nafsi yangu na mwili kwa damu ya Yesu. Amen!**

## 16. Kiwango Chako cha Nguvu za Mungu Zinazosababisha Matokeo Kinategemea Kiwango Chako cha Maombi

Kiwango Cha  nguvu za maombi ya Yabesi kilisababisha matokeo yaliyomshawishi Mungu kutoa majibu haraka ndio maana Yabesi alijibiwa yale aliyoyaomba *'Kuomba*

*kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii (Yakobo 5:16 )".* Bidii ya maombi ya Yabesi ilisababisha matokeo lakini pia matokeo hayo yalitokana na kutokujikatia tamaa yaani kuomba bila kukataa tamaa. Yesu anawambia wanafunzi kupitia dokta mmoja anayeitwa *Luka 18:1; Akawaambia mfano, ya kwamba imewapasa kumwomba Mungu sikuzote, wala wasikate tamaa.*

Siri zote za nguvu za Mungu zipo kwenye maombi. Ngoja nikushuhudie; niliwahi kufunga siku 7 kavu; mfungo wangu wa kwanza nikiwa Mwanza Bwiru--Jiwe kuu nikiwa pangoni. Baada ya mfungo huo nilijiona nina upako kiasi cha kutamka tu mambo yanatokea, nzuri zaidi nilienda kuhubiri injili Magu sehemu moja inaitwa Ngasamo. Nguvu za Mungu nilizishangaa sana kuona mapepo, majini, mizimu na wenye magonjwa kama viziwi wakipona! Tangu siku hiyo maombi niliyaheshimu sana.

Ndiyo maana ukikaa kwenye maombi muda mrefu nguvu za Mungu huongezeka. Kama wewe ni mtumishi na unataka Mungu akutumie kwa viwango vya juu, mapepo yawatoke watu, viwete watembee, viziwi wasikie, lakini hutaki maombi, maana yake utabakiza tu maneno. Ukweli ni kwamba, "**Nguvu za Mungu zinatoka kwenye maombi"**

## 17: "Nawe Ungenilinda na Uovu"

"...*Nawe ungenilinda na uovu..."(1 Mambo ya Nyakati 4:10)*". Yabesi anaonesha alikuwa mawindo ya ibilisi. Sasa anaweka msimamo wake binafsi. Sasa unilinde na ibilisi yaani usinitie tena katika majaribu. Yabesi alikuwa mateka, huwezi kusema ulindwe na ouvu kama hauko kwenye uovu. Maana yake Yabesi alikuwa gereza la uovu na mateka *.Lakini watu hawa ni watu walioibiwa na kutekwa; wote wamenaswa katika mashimo, wamefichwa katika magereza; wamekuwa mawindo, wala hapana aokoaye; wamekuwa mateka, wala hapana asemaye, Rudisha (Isaya 42:2*2 )".

Ashukuriwe Mungu aliyemtoa Yabesi kwenye umateka! Nawe leo Yesu akutoe kwenye uovu wa kishetani kwa jina la Yesu. Yabesi alikataa maroho ya mabalaa, mikosi, nuksi na laana. Yabesi aliomba kuondolewa kisilani, magonjwa na mambo yanayosababisha apatwe na maovu. Ngoja nikupe mfano; umewahi kujiuliza kwa nini watu wengi kuna miezi huwa wanasema; huu mwezi ajali nyingi hutokea? Au siku katika wiki; siku fulani huwa siyo nzuri kwa nini? Au miezi fulani huwa tunaugua sana.

Umewahi kujiuliza kwa nini? Kama mwombaji shetani hukamata lango la muda kuachilia uovu wake. Sasa usipoomba juu ya hayo malango ya siku, miezi au miaka, shetani ataachilia uovu wake! Kama mwombaji mweke Yesu kwenye hayo malango

yako ili akulinde na uovu kwa kutamka *Zaburi 24:7-10. Inueni vichwa vyenu,* ***enyi malango,*** *Inukeni, enyi malango ya milele, Mfalme wa utukufu apate kuingia.*

Ni nani Mfalme wa utukufu? BWANA mwenye nguvu, hodari, BWANA hodari wa vita. *Inueni vichwa vyenu, enyi* ***malango,*** *Naam, viinueni, enyi malango ya milele, Mfalme wa utukufu apate kuingia. Ni nani huyu Mfalme wa utukufu? BWANA wa majeshi, Yeye ndiye Mfalme wa utukufu.*

**UKIRI: Ee Mungu Baba nimekuwa mateka na mawindo ya ibilisi kwa kujiingiza mwenyewe au kwa kuingizwa na ndugu, naomba damu Yako initakase na udhalimu wote uliofanyika nami usinitie majaribuni bali niokoe na yule mwovu siku zote za maisha yangu. Amen!**

## 18. "Ili Usiwe Kwa Huzuni Yangu"

***"…****Ili usiwe kwa huzuni yangu!... (1 Mambo ya Nyakati 4:10)".* Aliombal ili Mungu amwondolee huzuni, japo Yabesi alizaliwa katika Mateso na huzuni, huzuni yake iligeuka kuwa furaha, kama Yohana anavyosema; ninyi mtahuzunishwa, lakini huzuni yenu itageuka kuwa furaha. Mungu alisikia maombi ya Yabesi na kumpa furaha. Haijalishi umekuwa mtu wa machozi kama nabii wa machozi. Yeremia aliwahi kusema ,nalitoka tumboni kwa sababu gani, kuona taabu na huzuni, hata siku zangu ziharibike katika aibu? Mungu akupe furaha, Yesu alikuja ulimweguni kuchukua huzuni zetu, yeye hakika ameyachukua masikitiko yetu na amejitwika huzuni zetu. Kwa nini uhuzunike mpendwa? Maana Biblia inasema; heri wenye huzuni; maana hao watafarijika. Yabesi alikataa huzuni kwa njia ya maombi nawe leo kataa huzuni kwa jina la Yesu.

**UKIRI: Ee Mungu nisamehe kwa kujilaani mimi mwenyewe na kusababisha huzuni na uchungu. Nakataa huzuni ya kifamilia kwa jina la Yesu, nakataa roho ya huzuni na kulia katika jina la Yesu. Unirudishie furaha ya wokovu wako; Unitegemeze kwa roho ya wepesi katika Jina la Yesu Amina.**

## 19. Jifunze Kuwaombea na Wengine

Unaweza ukaniuliza swali; Malosha, kwani Yabesi aliwaombea wengine? Jibu ni hapana alijiombea yeye kwanza Ili atengeneze ushuhuda wa kuwaombea wengine! Mfano, huwezi kuwaombea watu wapate magari wakati wewe hata baiskeli huna. Ili watu waone ushuhuda wao kuamini kile unachowaombea, mwombe Mungu akufanikishe kwanza wewe! Najua una swali, na swali lako ni hili: Je, nisipovuka ina

maana sitawaombea wenzangu? Jibu ni hapana! Uvuke au usivuke ni shariti uwaombee wengine.

**Kutokuwaombea wengine ni dhambi:** Unasema, umejuaje? Mzee Samweli anasema "*Walakini mimi, hasha! Nisimtende BWANA* ***dhambi*** *kwa kuacha kuwaombea ninyi; lakini nitawaelimisha katika njia iliyo njema, na kunyoka ( 1 Samweli 12:23)"*. Umeona? Ndiyo maana ni muhimu kuomba toba kwa kutokuwaombea wengine. Musa aliwaombea Israeli, Yeftha aliomba juu ya Israeli kama mwamuzi wa Israeli. Epafraditho aliombea kanisa la kwanza walipokuwa na ghasia. Kanisa la kwanza walimwombea Petro alipokuwa gerezani.

**Kuwaombea wengine kunaondoa uteka (vifungo):** Usiangalie mambo Yako mwenyewe angalia na mambo ya wengine. Ayubu alipowaombea watu nini kilitokea? Mungu aliondoa uteka juu yake! "*Kisha BWANA akaugeuza uteka wa Ayubu, hapo alipowaombea rafiki zake; BWANA naye akampa Ayubu mara mbili kuliko hayo aliyokuwa nayo kwanza Ayubu 42:10)*". Swali langu ni hili: Je, unawaombea wengine? Ukiwaombea wengine Mungu atashughulika na mambo yako. Katika dhambi inayolitesa kanisa mpaka sasa ni **UNAFIKI.** Watu wako tayari kukusifia na kukutia moyo na kukuambia, mtumishi tunakuombea usiwe na wasiwasi, kumbe moyoni wanasema, 'ayaah! nimwombee kanipa nini?, kila mtu ajue mzigo wake'. Ni mara ngapi unawasema watumishi wa Mungu? Wengine mpaka wamediliki kuwaroga lakini wamegonga mwamba! Wewe waombee tu, kama Mungu amekupa hiyo neema waombee tu, kwa maana maandiko yanasema, "*Basi imetupasa sisi tulio na nguvu kuuchukua udhaifu wao wasio na nguvu, wala haitupasi kujipendeza wenyewe (Warumi 15:1)*". Kuchukua udhaifu ni kuwaombea na wala siyo kuwasema!

**Ukiwaombea wengine uwe tayari kukutana na jaribu juu ya kile unachokiombea:** Najua hujanielewa. Ukiombea mtu, Mungu atakupa jaribu juu ya hicho unachokiombea kama kweli unao mzigo wa kuomba juu ya hicho kitu. Ngoja nikupe mfano; dada mmoja aliniomba nimwombee Ili aolewe. Kumbuka hapo mimi sijaoa bado. Jaribu nililolipata juu ya yule dada ni aliniuliza hivi: 'mtumishi, Mungu amekuonesha nani?' Nikamwambia, kiukweli nimeona unanisumbua tu dada yangu kukuombea maana tayari una mtu ila unataka tu kuhakiki!

Yule dada alicheka kweli halafu akasema ni wewe mtumishi uko moyoni mwangu! Duh! Nilishituka nikakumbuka Yusufu na mke wa Potifa na Amnoni na Tamari. Nikamwambia kama kweli niko moyoni mwako piga magoti nikuombee. Akapiga magoti nikamwombea, na kabla sijaanza mapepo yalilipuka ya mahaba yanasema "tulikuwa tunakujaribu kama unapenda ngono kumbe hupendi hahahahahaha!". Mapepo yalicheka kweli kweli nikayakemea 'Kwa jina la Mfalme Yesu ukawe huru.'

Fikiria kitu kama hicho mtu unamwombea kumbe anakutaka kimapenzi. Niliwaza sana kumbe unaweza kuwa unahubiri kuna mtu 'kakuzimia, kafa, kaoza'. Kwa jina la Yesu ushindwe na ufe na siyo ulegee, ndiyo maana Sulemani alipoomba hekima Mungu alimpa jaribu juu ya kile alichokiomba! Juu ya kuamua kesi ya wale makahaba wawili waliolalia mtoto mmoja mwanae akafa na kweli aliamua vizuri maana aliomba hekima *(1 Wafalme 3:16-28) Na Israeli wote wakapata habari za hukumu ile aliyoihukumu mfalme wakamwogopa mfalme; maana waliona ya kuwa hekima ya Mungu ilikuwa ndani yake, ili afanye hukumu.*

---

# SURA YA TATU

---

## Maswali Yako ni Yapi Kwa Mungu? Majibu ya Mungu ni Yapi Kwako?

## Maswali Yako Kwa Mungu

## 20. "Naye Mungu Akamujalia Hayo Aliyoyaomba"

"*..Naye Mungu akamjalia hayo Aliyoyaomba (1 Mambo ya Nyakati 4:10)"*. Yabesi alipewa majibu ya maombi yake. '**Shetani hakuzuii kuomba atakuzuia usipate majibu ya maombi yako',** ndiyo maana ni muhimu sana unapomaliza kuomba zungushia moto, damu ya Yesu na kukataa visasi na visilani vya shetani juu ya maombi yako. Yabesi alipomulingana Mungu wa Israeli alipoomba alienda na agenda muhimu mbele za Mungu na akiambatanisha na maswali. Na haya maswali kila mwombaji anapoenda mbele za Mungu sharti awe nayo ili Mungu akujalie hayo unayoyaomba kama Yabesi.

**(i) Kwa nini (Why?)**: Unapokuwa kwenye maombi hili ni swali kwa Mungu kutaka sababu ya wewe kuwa hivyo. Yabesi aliuliza, kwa nini mimi tu huzuni kila siku? Kwa nini sijaona mkono wako? Kwa nini mipaka imefungwa? Kwa nini uovu umenisonga? Je umewahi kumuuliza Mungu swali kama Hilo? Kwamba kwa nini sijaolewa? Kwa Nini natesaka na ugonjwa? 'Kwa nini? Kwa nini? Kwa nini?' Hebu jaribu kufanya hivyo uwe na uhakika kuwa utapewa sababu ya kile ulichouliza. Kwa njia mbali mbali--kwa maono, ndoto, na Neno la Mungu, na kwa matukio atakusemesha. Kwa njia tofauti tofauti na ujifunze jinsi ya kusikia kutoka kwa Mungu. Kwa njia ya Maombi na kuona vitu katika ulimwengu wa Roho. Ni kwa njia ya Maombi! Unapouliza hivyo KWA NINI? Mungu anaweza kukuambia tatizo lako na unapomaliza maombi usiwahi kutoka kwenye maombi. Kuna kitu Mungu atakusemesha; anaweza kusema na wewe kama ni kuomba toba juu ya dhambi zako, au kuambatanisha maombi yako na sadaka! Au akakwambia nakupitisha kwenye shule ya majaribu kama Ayubu! Na hapa ni muhimu kuombea macho ya rohoni yaone vizuri, na masikio ya rohoni yasikie vyema.

**(ii) Lini (When?):** Uwe na uhakika. Yabesi aliuliza, lini Mungu utaniondolea haya mateso? Habakuki pia alimuuliza Mungu swali hili, kwamba, Ee Bwana nilie hata lini? Hili swali linalenga **Muda.** Kwamba ni kwa muda gani sasa nitakuwa huru? Lini nitapona? Lini nitakwenda Marekani? Lini utanipa mtoto? Lini nitanunua gari? Lini mume wangu atabadilika? 'Lini? Lini? Lini?'. Yabesi alijaliwa hayo aliyoyaomba na Mungu alimjibu hayo aliyoyaomba. Mungu wetu hakawii wala hachelewi na ahadi zake ni za kweli. Kwenye hili swali wakristo wengi tumewapoteza, wengine wamekata tamaa na kwenda kuuliza kwa miungu mingine, baada ya kukosa muda gani tatizo litaisha.

**(iii) Wapi (Where?):** Hili ni swali muhimu la kutaka kujua 'eneo muujiza' wako utafanyikia. Yabesi muujiza wake ulifanyikia Yuda huko huko! Je, wewe unauliza kwa Mungu hivi wapi nitaolewa? Ni Rwanda au Burundi? Ni wapi huduma yangu itainuliwa? Ni hapa Tanzania au Ulaya? Wapi nitapona huu ugonjwa? Mungu anaweza

kukuambia utaponea hapa hapa kanisani--kuna mtumishi atakuja kuhubiri na huyo atakuponya. Namani hakujua ataponea wapi ukoma wake lakini aliponywa na nabii kutoka Samari. Swali langu ni hili: Kwani Yuda hakuwa na manabii? Kwani Babeli hakuwa na watu? Tena huyo nabii alimpa tu maelekezo na Namani akaponea mto Yordani! Usidharau eneo la muujiza maana Neno jema laweza kutoka hapo, hapo kanisani unaposali.

Usidharau eti hawana upako--hapo hapo unapopadharau ndipo panakutoa jangwani kwenda kanaani yako. Baba yangu ni mchungaji lakini sikuwahi kuokoka! Mpaka pale nilipoamua kukiri kwa kinywa changu kwenye mkutano mmoja wa Moses Kulola pale Viwanja vya Furahisha. Fikria nilikuwa sijaokoka na ni mtoto wa Mchungaji! Nikajifunza kitu, **'kumbe kuna kujiunga na kuokoka'** na 'k**una kuokoka na kuokotwa'**. Unaweza ukawa ni mtoto wa mtumishi ila hujaokoka, lakini uko kwa waliookoka--ila hujaokoka kama akina Hofini na Finehasi watoto wa kuhani Eli. Msalishe sala ya toba mwanao ya kumkubali Yesu kama Bwana na Mwokozi wa maisha yake. Kwa hiyo, mahali ambapo sikutarajia ndipo nilipompokea Bwana Yesu! Je, unajiuliza nitaokokea wapi? Kama hujaokoka, okoka humu humu, kwa sababu saa ya wokovu ni sasa. Wakati ukiendelea kusoma kitabu hiki, sema sala hii:

**Sala ya toba: Ee Mungu, mimi ni mwenye dhambi natubu dhambi zangu zote kwa kumaanisha kuziacha, futa jina langu kwenye kitabu cha hukumu; andika jina langu kwenye kitabu cha uzima. Nipe nguvu za kushinda dhambi. Karibu Roho Mtakatifu uniongoze siku zote za maisha yangu. Ahsante kwa kuniokoa katika jina la Yesu Kristo! Amina**!

## Majibu Yako Kwa Mungu

Yabesi alipouliza hayo maswali **kwa nini, lini na wap**i uwe na uhakika Mungu alimujibu majibu matatu tu nayo ni N**diyo, Hapana, Subir**i mojawapo ya haya majibu ndiyo na sisi tunapoomba tunajibiwa mojawapo. Majibu ya Mungu ni haya:

**(i) Ndiyo**

**(ii) Hapana**

**(iii) Subiri**

Yabesi Mungu alimujalia hayo aliyoyaomba, kwa maana ya kupata jibu mojawapo kati ya hayo ambalo ni **NDIYO**.Ukiuliza hayo maswali matatu kwenye maombi na Mungu atakupa jibu mojawapo kati ya hayo matatu; Ndiyo, Subiri na Hapana.

Kama Mungu alimjalia yale aliyoyaomba ina maana alipata haki yake! Swali; Kwa wewe msomaji wangu, kama Yabesi alipata aliyoyaomba, je, aliendelea na maombi tena? Je! Unapoomba Mungu akakujibu, je unaendelea na kuomba tena? Je, umeomba mke umepata, je unaomba tena? Au unamsahau Mungu kabisa? Musa anawambia Wana wa Israeli kwamba, 'Jihadhari, usije ukamsahau BWANA, Mungu wako, kwa kutozishika amri zake, na hukumu zake, na sheria zake, ninazokuamuru leo,basi hapo moyo wako usiinuke, ukamsahau BWANA, Mungu wako, aliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa'; unapojibiwa maombi usiache kuomba. Biblia imenyamaza kimya kama Yabesi aliendelea na maombi. Muujiza wako unalindwa na maombi. Kumbuka hili usije ukasahau "**Ulichokipata kwenye maombi kinalindwa na maombi".**